

## **Mkengeuko wa Malezi kwa Wahusika katika Riwaya ya *Rosa Mistika***

*Selestino H. Msigala*<sup>1</sup>

### **Ikisiri**

Makala hii imechunguza mkengeuko wa malezi wa wahusika katika riwaya ya *Rosa Mistika*. Data za makala zimepatikana maktabani kwa mbinu ya usomaji makini wa matini ya riwaya husika na kisha kuchambua data hizo kwa mkabala wa kimaudhui na kuziwasilisha kwa mkabala wa kitaamuli. Makala imeongozwa na misingi ya Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi katika ukusanyaji na uchambuzi wa data. Matokeo yanaonesha kuwapo kwa matukio mengi ya wahusika kukengeuka malezi katika riwaya hii. Matukio hayo ni ubakaji, kujiua, rushwa, umalaya, kupuuzwa ushauri na matusi. Matukio haya yameoneshwa katika kazi husika kwa kuwa ni mwakiso wa uhalisi wa kijamii kama Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi inavyofungamanisha jamii na kazi za fasihi.

### **1.0 Utangulizi**

Malezi ni jambo muhimu kwa ustawi wa jamii yoyote kwani hutarajiwa kutoa maadili<sup>2</sup> yaliyo kama dira katika maisha ya kijamii (Mbatiah, 2012; Wanjala, 2015; Beebee, 2016). Mathalani, Wanjala (2015) anaeleza jinsi malezi kwa wahusika yanavyoathiri utambulisho wa vijana katika riwaya ya Kiswahili. Mawazo yake yanaonesha kuwa ili vijana wapate maadili ya jamii zao, wanapaswa kupata malezi yanayofaa kupitia taasisi mbalimbali katika jamii kama vile familia, dini, shule na vyuo. Kwa upande mwingine, Beebee (2016) anafafanua kuwa maadili wanayopewa wahusika wanaotumika katika riwaya huwaongoza wasomaji katika mwelekeo ulio bora kutokana na malezi ya jamii.

TUKI (2014) inafafanua kuwa malezi ni njia ya ukuzaji wa mtoto kwa kufuata tabia na mwenendo unaostahiki. Nalo BAKIZA (2017) linaeleza kuwa malezi ni mafundisho mazuri yanayotolewa na mzazi au mlezi katika makuzi ya mtoto. Wapokeaji na watoaji wa maelekezo ya kimalezi wanapokiuka kutoa au kupokea maelekezo ya kimalezi husababisha kinachotarajiwa katika malezi hayo.

---

<sup>1</sup>Mhadhiri Msaidizi, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.  
Baruapepe: selestinomsgala@gmail.com

<sup>2</sup>BAKIZA (2010) linafafanua kuwa maadili ni mwenendo unaokubalika katika jamii fulani; mafunzo ambayo yanahusu mwenendo mwema.

kutofikiwa. Hali hii katika makala hii ndiyo inatazamwa kama mkengeuko wa malezi

Kila kundi la wanajamii huhitajika kuwa na malezi yanayokubalika ili kuondoa migogoro na changamoto mbalimbali (Mayaka, 1991; Diegner, 2002; Mahonge, 2016). Mlacha (1986) anafafanua kuwa wahusika wanaotumika katika kazi za nathari za Kiswahili mara nyingi huwa vijana ambao ni wapya katika jamii zao. Kwa upande mwingine, vijana hao huwa katika umri wa kuanza kujitegemea, kujenga familia zao na huwa tayari kupata watoto. Vijana hao hujitenga na jamii zao kutokana na kuwa katika umri wa kutaka uhuru wa kujitegemea katika maamuzi. Aidha, wapo vijana wengine ambao wamepata utamaduni wa kigeni kupitia elimu ya Kimagharibi ambao ni tofauti na utamaduni wao asilia. Utamaduni huo wa kigeni unaonekana kuwa tofauti na utamaduni asilia wa jamii na hivyo kusababisha mgogoro wa malezi katika jamii.

Mawazo ya Mlacha (1986) yanabainisha migogoro miwili ya kimalezi. Kwanza, kuna mgogoro kati ya wahusika vijana na wahusika wazazi. Mgogoro huu unatokana na wahusika vijana kutafuta uhuru wao hasa baada ya kujiona kuwa nao ni watu wazima na wanastahili kujitegemea kwa kuanzisha familia zao au kuwa huru kujiamulia kufanya mambo watakayo kwa upande mmoja; na kwa upande wa pili, jamii nayo inataka vijana hao waingie kuwa sehemu yao na kufuata mwongozo wa jamii. Mgogoro wa pili wa kimalezi unaoibuka ni ule wa wahusika vijana wanaopata athari ya utamaduni wa kigeni. Utamaduni huu wa kigeni kwa kiwango kikubwa wanaupata kupitia elimu ya kigeni. Elimu hii ya kigeni inawafanya vijana kupata upya wa malezi tofauti na malezi ya awali yaliyopo katika jamii zao. Wahusika hawa vijana waliopata malezi ya kigeni wanajikuta kutoelewanana jamii kwa ujumla, wakiwamo pia vijana wenzao katika jamii.

Mawazo ya Mlacha (1986) yanashadidiwa na Mayaka (1991) anayefafanua athari za elimu ya kikoloni katika kuwakengeusha vijana na hivyo kuzua migogoro katika jamii. Hata hivyo, kuwapo au kutokuwapo kwa elimu ya kikoloni na athari za Kimagharibi si kigezo pekee cha kuzua mgogoro wa kimalezi. Suala la wakati, umri na mazingira ya kijamii ni kichocheo kimojawapo cha mvutano wa malezi katika jamii kati ya vijana na wazee.

Fauka ya hayo, wapo wataalamu wanaoona kuwa mazingira ya kijamii anayopitia mhusika huweza kumsukuma kufikia hatua ya kuyakengeuka malezi (McCall, 1981; Plomin na Ausbury, 2005; Bownlee, 2006; Durisic na Bunijevac, 2017). Mathalani, Wamitila (2008) na Madumulla (2009) wanadokeza mkengeuko wa wahusika katika aina za riwaya za Kiswahili wanazozijadili. Wamitila (2008) anapoelezea aina za riwaya, anagusia riwaya ya ukuaji. Anafafanua kuwa riwaya ya aina hii hujifunga kwenye maisha ya mhusika ambaye anachunguzwa tangu utotoni au ujanani hadi utu uzima. Maisha ya mhusika huyo huchunguzwa sambamba na jinsi asasi tofauti zinavyoathiri maisha yake. Malezi anayoyapata ama kuyakosa mhusika huyo katika mazingira anamokulia yanaweza kuathiri

maisha yake ya baadaye. Maelezo ya Wamitila (2008) yanadokeza mambo mawili: kwanza, yanaeleza kuhusu wahusika kupata malezi yasiyotarajiwa na au kuyakosa kabisa malezi yanayostahili. Pili, nafasi ya mazingira anamokulia mhusika kama vile nyumbani, shuleni, chuoni na kazini yanaweza kuwa na mchango katika malezi ya mhusika. Hata hivyo, Wamitila (2008) haoneshini mambo gani ya mkengeuko wa malezi yanayofanywa na wahusika, jambo ambalo lilisukuma utafiti wa makala hii kufanyika.

Mkengeuko wa malezi unaweza kusawiriwa katika kazi za fasihi, ikiwamo riwaya. Kwa mfano, Mbatiah (2012) anaitazama riwaya kama tahakiki ya jamii. Yeye anaonesha namna mwandishi wa riwaya anavyoandika kukidhi mahitaji ya jamii anayoiandikia. Hii ina maana kuwa kwa kutumia riwaya, jamii huweza kutazama mwenendo wake. Hata hivyo, ingawa malezi hutolewa kupitia kazi mbalimbali za fasihi, bado baadhi ya wahusika wanaotumiwa katika kazi za fasihi ikiwamo riwaya huchorwa kuyakengeuka malezi hayo (Mlacha, 1986; Mayaka, 1991; Wamitila, 2008 na Madumula, 2009). Kwa mfano, Mayaka (1991) anapotafiti ukengeushi wa wahusika wasomi katika riwaya za Euphrase Kezilahabi anaonesha ni kwa namna gani wahusika vijana wanakengeuka misingi ya jamii zao na hivyo kuleta migogoro katika jamii zao. Ukengeukaji wa malezi unaweza kusawiriwa katika kazi za fasihi kwa sababu fasihi ni zao la jamii, hivyo, yote yanayotokea katika jamii husika huweza kuonekana katika kazi mbalimbali za fasihi (Dubey, 2013; Nworah na Eziafa, 2014; Duran, 2015; Mulokozi, 2017).

Mjadala wa hapo juu ukichunguzwa, inabainika kuwa ingawa wahusika hukengeuka malezi, wataalamu na wachambuzi hutofautiana katika kuelezea jambo hili. Wapo wanaoona kuwa kukengeuka malezi kwa wahusika katika kazi za fasihi kunasababishwa na wazazi au walezi (Belsky, 1984; Mitchell, 2010; Salaria, Wells na Sarkadi, 2014; Wanjala, 2015; Mbatiah, 2016; Doepke na Zilibotti, 2019). Kwa upande mwingine, wapo wataalamu wanaoona kuwa baadhi ya wazazi na walezi huwatupia lawama watoto wao kuwa wanabadilika hasa wanapotoka mikononi mwao na kuingia katika jamii kutokana na kushindwa au kupuuza malezi na maelekezo kutoka kwa wazazi au walezi wao (Joseph, 1994; Diegner, 2002; Ondieki, 2015; Jonas, 2017). Aidha, upande mwingine jamii hulaumiwa kwa kushindwa kuendeleza malezi yanayofaa kutoka kwa wazazi au walezi wa watoto (Belsky, 1984; Curzer, 1996; Bownlee, 2006; Mitchell, 2010; Martin, 2017; Sanga, 2018). Tofauti hizi za kimtazamo ndizo zilizosukuma kuandikwa kwa makala hii. Kwa hiyo, makala hii inakusudia kujadili mkengeuko huo wa malezi kwa kutumia wahusika wa riwaya ya *Rosa Mistika* (Kezilahabi, 1971).

## 2.0 Vyanzo vya Data

Data zilizotumiwa katika makala hii zimekusanywa kwa njia ya mapitio ya nyaraka za maktabani pamoja na udurusu wa matini ya riwaya husika ya *Rosa Mistika*. Riwaya hii imeteuliwa kwa kuzingatia uchunguzi wa awali uliobaini

kuwa ni riwaya ya kiuhalisia<sup>3</sup>, katika mkondo wa riwaya za ukuaji ambazo zinamwonesha mhusika tangu akiwa mdogo hadi mtu mzima. Riwaya hii pia imeonesha kuwa na kiwango kikubwa cha wahusika wanaokengeuka malezi.

### 3.0 Msingi wa Nadharia

Uchambuzi wa data za makala hii umeongozwa na misingi ya Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi. Nadharia hii imeteuliwa kwa sababu inashikamanisha masuala ya jamii na kazi za fasihi. Nadharia hii inaelezwa na Coser (1963) kuwa iliasisiwa na Charles Taylor (1822-1917) na Georg Lukacs (1885-1971). Kwa mujibu wa nadharia hii, fasihi na sanaa ni picha ya uhalisia katika jamii ambamo kazi husika imeibuka. Hivyo, nadharia hii inalenga kuonesha uhusiano uliopo kati ya fasihi na jamii. Hii ni kwa sababu fasihi siku zote huzaliwa katika mazingira ya kijamii. Kwa namna nyingine, Hellen (1966) akieleza kuhusu fasihi na jamii kama Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi inavyofafanua, anadai kuwa fasihi ni taswira, mwongozo na kishawishi cha mabadiliko katika jamii. Misukumo na mahitaji ya mabadiliko katika jamii huchagizwa na fasihi ambayo huisaidia kukua. Katika mwelekeo wa ushawishi, fasihi hujikita katika kuonesha mielekeo na tabia za watu katika njia mbalimbali (Chatterjee 1988; Titus, 2018). Tukiisoma na kuichambua kazi ya fasihi tunaweza kupata picha halisi ya jamii husika (Carter na Carter, 2014).

Kupitia wataalamu hao walioelezwa hapo juu, misingi ya Nadharia ya Kisosholojia ya Fasihi ifuatayo inabainika: kwanza, binadamu ni uti wa mgongo wa sanaa na ulimwengu kwa ujumla. Hivyo, kazi yoyote ya fasihi ni taswira ya kijiografia, kimazingira na kitamaduni ambamo kazi hiyo imezuka. Kwa namna hiyo, kazi hiyo haipaswi kutenganishwa na muktadha kwa kuwa hufungamana na historia ya jamii. Pili, fasihi ni dhihirisho la ujumi na ubunifu wa jamii katika kupambana na mazingira yake, na hivyo haiwezi kutenganishwa na harakati za binadamu zinazoongoza maisha. Tatu, usuluhishi wa migogoro unaosawiriwa ndani ya fasihi kama vile katika msukumo wa matukio unaficha migongano anuwai ya kijamii ambayo haijasuluhishwa. Nne, mhakiki hawezi kuhakiki kazi ya fasihi bila kuzingatia miktadha yake (mazingira, wakati na maisha ya mwandishi). Kama ilivyoelezwa hapo awali, nadharia hii imesaidia ukusanyaji na uchambuzi wa data za riwaya ya *Rosa Mistika* (Kezilahabi, 1971).

### 4.0 Mkengeuko wa Malezi katika Riwaya ya *Rosa Mistika*

*Rosa Mistika* ni riwaya ya kihalisia iliyoandikwa na Euphrase Kezilahabi mwaka 1971. Simulizi ya riwaya ya *Rosa Mistika* imejengwa kwa mhusika Rosa Mistika na familia yake ya baba Zakaria, mama Regina na wadogo zake: Flora, Honorata,

<sup>3</sup>Riwaya ambazo huonesha mwelekeo mkubwa wa kuibua athari ya uhalisia au hali halisi kwa kusawiri wahusika kwa uchangamano na undani na wanaokitwa katika matabaka mahususi ya kijamii (Wamitila, 2008)

Stella, Sperantia na Emmanuel. Rosa analelewa kwa ukali, kutishwa na kupigwa na baba yake tangu akiwa shule ya msingi baada ya kugunduliwa kuwa anatongozwa na mvulana, Charles. Hali hii inafanya awaogope wavulana tangu akiwa mwanafunzi wa shule ya msingi. Hata hivyo, Rosa anabadilika na kuanza kuwa malaya baada ya kufika sekondari kwa kuwa baba yake na wanaomchunga hawapo tena; anajiona yuko huru kufanya analolitaka. Kutokana na tabia ya umalaya, kutoroka usiku na kulala nje ya shule; Rosa anasimamishwa masomo na kuruhusiwa kwenda shuleni kufanya mtihani wa mwisho tu. Matokeo yanapotoka Rosa anapata ufaulu wa daraja la tatu uliomwezesha kujiunga na mafunzo ya ualimu chuoni Morogoro.

Akiwa chuoni Morogoro tunaoneshwa Rosa akiendeleza tabia ya umalaya na kila mwanamume aliyemtaka. Rosa anajihusisha kimapenzi na Thomas, Mkuu wa Chuo cha Morogoro. Wakati wa likizo Rosa anaendeleza umalaya kwa kuchukuliwa na Mkuu wa Wilaya, tukio linalomfanya baba yake kumkataa Rosa kuwa si mtoto wake, naye Rosa kumkataa baba yake. Rosa anarudi chuoni. Anafanikiwa kumaliza masomo ya ualimu na kupangiwa kufundisha katika mkoa wa Mwanza. Huko anaanza mahusiano ya kimapenzi na Charles na kukubaliana kuoana. Hata hivyo, uchumba wao unavunjika baada ya Rosa kukutwa si bikira; na Rosa anapogundua kuwa ameachwa na Charles kwa sababu yeye si bikira, anaamua kujiua.

Katika kuyajadili masuala ya mkengeuko wa malezi, mwandishi wa riwaya ametumia mbinu mbalimbali ikiwamo kuwajenga wahusika wanaokengeuka malezi. Kwa ujumla, riwaya imethibitisha kuwapo kwa mkengeuko wa malezi kwa wahusika ulioibuliwa na mwandishi kutoka katika jamii na tajiriba yake. Masuala mbalimbali yanayohusiana na mkengeuko wa malezi katika riwaya husika yamejadiliwa katika sehemu inayofuata.

#### **4.1 Ubakaji**

Domingo (1992) anafafanua kuwa ubakaji ni matumizi ya nguvu au ulazimishaji wa kuingiliana kimwili pasipo utayari. Pia, ni matumizi ya ushawishi wa aina yoyote ambapo upande mmojawapo unakosa utayari. Baker (1999) anaeleza kuwa ubakaji ni kitendo cha kuutawala kwa nguvu mwili wa mtu mwingine ili kuutumia kingono bila ya ridhaa yake. Williams (2015) anaeleza kuwa ubakaji hutokea ikiwa sehemu za siri, vidole au mikono ya mtu au kitu kigeni kilichotengenezwa kwa ajili hiyo kinazamishwa au kupenyezwa sehemu za siri au sehemu za haja kubwa kwa mhanga bila ridhaa yake. Anaendelea kueleza kuwa katika ubakaji, mhanga anaweza kuwa ni mtu ambaye hana uwezo wa kukataa kwa sababu mbalimbali kama vile: kuwa mdogo kiumri, hivyo, kukosa uwezo wa kukataa na kuwa katika urazini usio wa kawaida kwa kuchanganyikiwa, kuwa na msongo wa mawazo, kulewa, ugonjwa au kuwa katika hofu au ugonjwa wa akili.

Kutokana na maelezo ya wataalamu hapo juu, tunaweza kueleza kuwa ubakaji ni kitendo cha kumwingilia mtu kingono pasipo ridhaa yake au kuwa

katika hali isiyo ya urazini kama vile ugonjwa, ulevi au umri mdogo. Ubakaji unaweza kuhusisha matumizi ya nguvu, ushawishi au kumfanya mhanga kuwa katika hali isiyo ya kawaida kwa dawa za kulevya, hofu, pombe au ahadi ya uongo ya kumuoa. Katika riwaya ya *Rosa Mistika* suala la mkengeuko wa malezi kwa ubakaji limejitokeza. Kwa mfano, mhusika Charles anamlewesha pombe Rosa na baadaye anambaka ili kuchunguza ikiwa Rosa ni bikira. Kupitia tukio hili la ubakaji ndipo Charles anagundua kuwa Rosa si bikira, hivyo, anatengeneza mpango wa kumwacha. Mwandishi anaeleza:

Bila shaka Rosa amelewa sana; sidhani kwamba ataweza kujitambua kesho. Sidhani kwamba yumo katika hali ya kuweza kunizuia. Nafikiri huu ndiyo wakati wa kuweza kuhakikisha. Alifika kitandani, alimshika Rosa, alimshika kichwa chake, alitikisa kwa nguvu, Rosa! Rosa! Amka! Amka! Rosa alikuwa amelala fofofu.... Aliona alikuwa amepoteza fahamu zake zote. Alivua nguo zake zote na baadaye alimvua nguo Rosa.... Rosa sasa alikuwa uchi.... Baada ya muda, Charles alionekana akijipangusa jasho. Baada ya kujipangusa jasho alionekana akimbeba Rosa kutoka kitandani. Alimlaza chini juu ya sakafu na kumwosha. Alifanya hivi ili Rosa asije akatambua yaliyotokea baada ya kunywa....Giza lilikuwa limeingia Charles alipohakikisha kuwa Rosa alikuwa bikira au hapana (Kezilahabi, 1971:87-86).

Katika nukuu hiyo tunaona jinsi mhusika Charles anavyombaka Rosa baada ya kumlewesha pombe. Kupitia tukio hilo la ubakaji ndipo Charles anagundua kuwa Rosa hakuwa bikira. Tukio la kukutwa si bikira linamuondolea thamani Rosa. Anaonekana kuwa ni malaya, hivyo, hafai kuolewa. Hata hivyo, hatuelezwi ni kwa namna gani Charles aligundua kuwa Rosa hakuwa bikira. Ikiwa Charles aligundua kuwa Rosa hakuwa bikira, basi tunabaini kuwa Charles alikuwa na uzoefu katika mapenzi na alishawabikiri wanawake kadhaa, jambo lililomfanya kuwa na uzoefu wa kutambua mwanamke yupi ni bikira na yupi si bikira. Kwa ufahamu huo, hata Charles naye alikuwa malaya na hivyo alipaswa kulaumiwa, jambo ambalo jamii ya mwandishi wa riwaya hii haioneshi kulifanya.

#### **4.2Kujiua**

Kujiua ni kitendo cha kujisababishia kifo kwa mtu mwenyewe (Seaver, 2009). Katika utafiti huu tunaweza kueleza kuwa kujiua ni kitendo cha kujitoa uhai. Katika riwaya ya *Rosa Mistika* wahusika wameonekana kukengeuka malezi kwa kujiua wenyewe. Jambo hili halikubaliki katika jamii kwa kuwa huzua migogoro na taharuki katika jamii. Katika riwaya hii, mwandishi anamtumia mhusika Rosa ambaye anajiua kwa kunywa unga wa vipande vya chupa vilivyochanganywa na maji. Hapa mwandishi anaeleza:

Alichukua ile chupa na kuisagasaga juu ya jiwe. Baada ya kuisagasaga aliweka ule unga wa vipande vya chupa ndani ya glasi. Aliweka maji.

Rosa alifikiri kwanza kabla ya kunywa. Alitubu dhambi zake. Alitafuta karatasi nzuri sana halafu alijichanja mkononi na wembe. Damu ilitoka. Kwa damu hiyo aliandika maneno fulani juu ya karatasi. Alipomaliza kuandika maneno yake Rosa alivuta hasira yake. Alifikiri juu ya maisha. Mara moja alikunywa yale maji. Alilala juu ya kitanda cha Honorata. Polepole damu ilianza kumtoka mdomoni. Vile vipande vya chupa vilimkatakata kooni. Rosa alitema mate. Aliona damu. “Asante. Kifo njoo upesi” alisema. Baada ya muda mfupi Rosa alisikia maumivu makali sana tumboni. Muda mrefu haukupita Rosa alijiona ameanza kupoteza fahamu... Alisema maneno yake ya mwisho. Hapakuwa na mtu yeyote aliyesikia ... Honorata alipokuja kumpasha habari juu ya kifo cha wazazi wao alifikiri Rosa alikuwa amelala. Rosa hakujitingisha. Honorata alitambua kuwa Rosa alikuwa hapumui. Alitambua kuwa Rosa alikuwa amekufa: mwili wake ulikuwa baridi. Honorata alianguka chini na kuzimia (Kezilahabi, 1971:90-91).

Nukuu hiyo inatuonesha namna mhusika Rosa anavyokengeuka malezi kwa kuamua kujiua mwenyewe. Rosa anajiua kwa kumkosa mwanamume aliyekuwa anampaenda, Charles, kwa sababu tu hakukutwa bikira. Mwandishi anataka kutuonesha kuwa katika jamii zetu wapo watu wanaoamua kujiua kwa sababu ya mapenzi kama alivyofanya Rosa. Jambo hili linaisukuma jamii mbele kufikiri ukubwa wa tatizo la kujiua kutokana na sababu za mapenzi. Hali hii huiwezesha jamii kutafuta mbinu mbadala za kutatua changamoto za kimapenzi badala ya kujiua kunakoweza kufanywa na wanajamii.

### 4.3 Rushwa

Shleifer na Vishny (1993) wanaeleza kuwa rushwa ni uuzaji wa huduma halali au vifaa vya serikali kwa ajili ya manufaa binafsi. Makala hii inaunga mkono maelezo ya Harrison (2007) anayeeleza kuwa rushwa ni matumizi ya mambo ya ofisi ya umma au mamlaka yoyote iliyoaminiwa kwa manufaa binafsi. Katika riwaya ya *Rosa Mistika* suala la mkengeuko wa malezi kupitia rushwa limeoneshwa kwa namna mbalimbali. Kwa mfano, tunaoneshwa mhusika Rosa ambaye ni mwanachuo akifanya ngono na Thomas ambaye ni mkuu wake wa chuo. Kutokana na mahusiano ya kingono na Mkuu wa Chuo, Rosa hafukuzwi chuo licha ya makosa ya umalaya aliyokuwa akifanya akiwa chuoni. Hapa mwandishi anaeleza:

Thomas alikuwa bado hajatoka kitandani Rosa alipomshika na kumrudisha. Rosa alimkumbatia Thomas. Thomas alikusanywa. Alivutwa. Aligusa mwili wa Rosa. Wakati huo Thomas alikuwa hafahamu yuko wapi. Alikuwa amekwisha kazi. Alisema maneno mengi. Aliapa yamini kwamba Rosa hatafukuzwa shule kamwe. Rosa aliona kwamba ameshinda (ameshinda kutofukuzwa masomo ya chuo). Sasa alikuwa akimpangusa jasho Mwalimu Mkuu wa Chuo: baada ya kujenga nchi mwananchi alitoka jasho (Kezilahabi, 1971:53-54).

Katika nukuu hiyo mwandishi anatuonesha ni kwa namna gani mhusika Thomas kama kiongozi mkubwa wa serikali aliyepewa jukumu la kuiongoza taasisi ya serikali anakengeuka malezi kwa kufanya rushwa ya ngono na anayemwongoza. Mhusika Thomas aliyepewa mamlaka na serikali kukiongoza Chuo cha Ualimu Morogoro anaoneshwa kufanya ngono na mwanafunzi wake Rosa. Kutokana na matendo hayo ya ngono, Thomas anashindwa kumfukuza chuo Rosa licha ya makosa ya kinidhamu aliyokuwa nayo. Rosa anafanikiwa kubaki chuoni kwa nguvu ya Mkuu wa Chuo, kwa sababu ya kutoa rushwa ya ngono. Mkengeuko wa rushwa ya kingono ni kinyume na malezi ya jamii na malezi ya kazi na ndiyo maana mwandishi ameamua kuibua jambo hili na kuliingiza katika kazi yake ili kuifanya jamii ichukue hatua ya mabadiliko.

#### 4.4 Umalaya

Umalaya ni utoji wa huduma ya mahusiano ya kingono kwa ajili ya kupata pesa, yaani kwa malipo; ni kitendo cha kuuza na kununua, kitendo cha kufanya ngono (Richard; 1979, Moen; 2014). Umalaya ni kazi ya kinyanyasaji na kinyanyapaaji kati ya kazi nyingi wazifanyazo wanawake, na ni kazi ya kinyume cha haki za mwanamke kwa kuwa inawageuza watu hao kuwa kama bidhaa kingono na kunyanyasika kiuchumi, kimwili na kisaikolojia na wengi wao huuawa (Farley, 1994; Iyer; 1998). Kwa hiyo, kutokana na maana hizo tunaweza kueleza kuwa umalaya ni tabia ya mtu kufanya ngono kama biashara au starehe yake na mtu ambaye hana uhusiano naye wa ndoa. Katika umalaya wa biashara aghalabu wanawake ndio huuza huduma ya ngono na wanaume hununua huduma hiyo (Iyer, 1998).

Katika riwaya ya *Rosa Mistika* mkengeuko wa malezi kupitia umalaya umebainishwa na mwandishi ili kuonesha namna jamii ilivyo katika changamoto hii ya malezi. Kwa mfano, katika riwaya hii mwandishi anamtumia mhusika Rosa ambaye kwa nyakati tofauti anaonekana kujihusisha na mapenzi na wanaume na wavulana wengi kwa ajili ya starehe zake. Wavulana wengi walionekana kwenda kujifunza kufanya mapenzi au kujifunza staili mpya ya kufanya mapenzi kwa Rosa. Wavulana hawa walienda kwa Rosa kwa kuwa alikuwa hakatai mvulana yeyote, pia alipenda kufanya nao ngono. Mwandishi anaonesha haya pale anapoeleza:

Rosa alilazwa hospitali mahututi kwa kutoa mimba ya miezi miwili. Wengine waliokuwa maskini katika mambo haya walianza kusema, “Labda bwana, inawezekana alikuwa na mimba, eti bwana!” Rosa alikaa hospitali kwa muda wa majuma mawili. Wavulana walimwomba apone upesi. Rosa alipona. Aliendelea na mchezo wake. Katika majuma mawili yaliyofuata Rosa alikonda sana, vijana walikuwa wakimzungumzia yeye katika vikundivikundi; hata yeye mwenyewe alifahamu. Alianza kuwa anaviziavizia vikundi hivyo ili afahamu wanasema nini juu yake. Siku hazikupita alipokuta vijana



wanaangalia gazeti. Alijificha. Alisikia maneno waliyokuwa wakisema. “Staili hii bado sijaitumia” “Kwanini bwana usiende Lab.” “Lab kwenyewe ni wapi?” Rosa alisikiliza mpaka mwisho wa mazungumzo yao. Kutokana na mazungumzo hayo, Rosa aliweza kuelewa kwamba walikuwa wamembandika jina la “Laboratory” yaani nyumba ya kufanyia majaribio. Rosa alitwa “Lab” kwa kifupi (Kezilahabi, 1971:45-46).

Katika dondoo hilo tunaoneshwa jinsi Rosa anavyokengeuka kwa kufanya umalaya ovyo na vijana wengi hadi kusababisha kupata mimba na kuzitoa. Rosa ananusurika kufa kwa kutoa mimba ya miezi miwili kwa siri japo baadaye kila mwanachuo anajua. Hata hivyo, licha ya kunusurika kufa Rosa anaendelea na mchezo wake wa kufanya umalaya. Kutokana na umalaya anaoufanyia, Rosa anapewa jina la utani *Laboratory*, yaani ‘chumba cha kufanyia majaribio’. Kila mvulana aliyetaka kufanya majaribio ya kufanya ngono alikwenda kwa Rosa na Rosa alimkubali kila mvulana. Rosa alikuwa malaya na wala hakujali. Kufanya umalaya Rosa kunamfanyia asikubalike katika jamii ya wanachuo wenzake. Hali ya kutokubalika kwa mtu anayefanya umalaya inaelezwa na Farley (1994) anaposema kuwa umalaya humfanyia mwanamke ajiharibu mwenyewe, asiaminike katika jamii, apoteze mawazo na msimamo wake, matamania yake na maadili yake. Kimsingi, makala hii imebaini kuwa Rosa hakuwa anapata mimba kwa bahati mbaya, alikuwa anakusudia kwa kuwa alikuwa akifanya umalaya na ndiyo maana kila alipokuwa akipata mimba alikuwa akiitoa. Kwa hiyo, alikuwa akifanya umalaya na hakuwa na hofu kuhusu mimba kwa kuwa alikuwa ana uhakika wa kuitoa pale atakapopata.

#### 4.5 Kupuuzwa Ushauri Mwema

Ushauri ni maneno ya kuwaongoza watu katika mienendo inayofaa; ni uongozaji wa kipi kinafaa na kipi hakifai kwa wakati na miktadha fulani (Curzer, 1996). Utoaji wa ushauri mwema ni jambo la msingi kwani huwasaidia watu wengine namna bora ya kuenenda hasa ushauri huo unapopokelewa na kutumiwa ifaavyo (Jonas, 2017). Inatarajiwa mtu anapopewa ushauri mwema autumie vizuri ili kumfanya abadilike na kujiona salama na kukubalika katika jamii. Hata hivyo, wapo watu ambao hupewa ushauri ili kutatua changamoto za hali walizonazo lakini wanapuuza kwa makusudi. Hali hii inawafanya waendeleo kuishi katika matatizo au changamoto zinazowafanya wasielewane na jamii inayowazunguka.

Katika riwaya hii, kwa mfano, mwandishi anamtumia mhusika Rosa kuonesha namna anavyopuuza ushauri tofauti kutoka vyanzo tofauti na hivyo kumfanyia aharibike kimalezi. Kwa mfano, mwandishi anamtumia mhusika Padri kwenda kumshauri Rosa. Mwandishi anaeleza:

Mimi mtumishi wa Mungu. Nimekuletea habari njema Rosa. Padri alifungua Biblia yake pale alipokuwa ameweka picha ya mtu msalabani... Alianza kumhubiria Rosa: “Usikate tamaa. Rosa usikate

tamaa. Kukata tama ni dhambi isiyoweza kuondolewa hapa duniani...Wokovu bado upo machoni mwako.” Rosa alianza kutapika maneno na matapishi hayamezwi tena. “Wokovu maana yake nini? Wokovu! Wokovu gani! Kama kuna moto basi nitakwenda!”... Padri, maisha yangu yamekwishakuharibika na sijali! Kwanini wewe ujali roho yangu kuliko mimi mwenyewe? Padri alimwanguka, alishangaa. Alisimama na kufungua mlango... Padre alionekana akitoka nje kasi sana na Biblia yake kwapani. Rosa alifunga mlango. Hakuzidi kumwona tena Padri huyo siku zilizofuata. Wakati huo Rosa alikuwa amekwishapata tabia ile ya kutojali watu wanasema nini. Yeye alijifahamu mwenyewe kuliko mtu yeyote. Mara nyingi alifanya mambo yaleyale walikuwa wakimzungumzia mbele ya haohao watu ili awakasirishe zaidi. Tangu siku hiyo mvulana yeyote aliyekua akiingia ndani ya chumba chake alitoka nje akipiga miayo moja kwa moja (Kezilahabi, 1971:49).

Katika dondoo hili tunaona namna Rosa anavyopuuza na kukataa ushauri wa kuchukua hatua ya mabadiliko kutoka kwa Padri. Rosa anashauriwa na kuaswa kubadilika katika matukio mbalimbali ya umalaya anayoyafanya; lakini anampuuza Padri na ushauri wake. Rosa anamkataa moja kwa moja pasipo kupepesa macho na kumfukuza Padri aliyekwenda kumshauri kuacha umalaya. Licha ya kumpa matumaini na uwezekano wa kubadilika, Rosa anapuuza na kukataa anachoshauriwa. Rosa anampinga Padri na kuendelea na umalaya wake akiwa na akili na uelewa timamu. Rosa anayafanya haya kwa sababu amekengeuka. Rosa hataki mtu yeyote yule kumshauri kwa sababu amebadilika kwa kukeuka malezi ya awali ambayo yalimuogofya kuhusu umalaya na athari zake. Anaona yeye yuko sawa na hataki mtu mwingine amshauri kuhusu yeye.

Katika jamii, watu wanaishi kwa kutegemeana na wanajamii wengine. Mtu mmoja pekee yake hajikamilishi katika maisha, huhitaji mtu mwingine ili kukamilishana (Cronin, 2006; Njogu na Chimerah, 2011). Ndiyo maana kwa kutambua jambo hilo, Padri anaamua kwenda kumshauri Rosa ambaye anakengeuka kwa kutosikiliza na kutotumia ushauri mwema anaopewa na Padri ili aweze kubadilika katika changamoto zake. Hali ya kupuuza ushauri inaelezwa na Jonas (2017) anayeona kuwa licha ya umuhimu wa ushauri, mara nyingine hutokea watoa ushauri kuwa katika mtanziko kwa ama kuogopa kuwapa ushauri watu kwa kuchelea kukataliwa au kubezwa kwa ushauri wao. Hali hii inapotokea, washauri hubaki katika mtanziko wa ama watoe ushauri au vinginevyo. Jambo hili ndilo linalomtokea mhusika Padri. Tunaoneshwa kuwa haridhishwi na namna Rosa alivyokataa ushauri na hivyo anaondoka na kutorudi tena. Padri haoni thamani ya kuendelea kumshauri Rosa kwa kuwa anaonekana kupuuza ushauri kwa makusudi.

Jambo jingine analolifanya Rosa kwa makusudi kabisa ni kuamua kuzidisha kufanya umalaya mbele za watu wanaomsema kuwa anafanya vibaya. Sasa Rosa anaamua kufanya ngono na kila mvulana anayeingia chumbani kwake

kwa kumshawishi ili kuwaonesha watu kuwa hajali mtu yeyote anayeweza kumshauri hata akiwa Padri. Kasi ya kufanya umalaya kwa Rosa inaongezeka baada ya Padri kwenda kumshauri. Rosa anafanya makusudi kuendeleza umalaya ili kuwaonesha wanaomshauri na wanaomsema kuwa hataki wala hawajali kwa kuwa wanamuingilia maisha yake aliyoyachagua. Rosa hataki kuingiliwa na mtu licha ya kuwa hicho anachokifanya hakikubaliki katika jamii anayoishi. Hali ya mtu kupuuza ushauri mwema kutoka kwa wanaojitolea kumshauri kwa manufaa yake, ni mkengeuko wa malezi kwa kuwa matokeo yake ni kuzua migogoro katika jamii ya wahusika kama ilivyokuwa kwa Rosa.

Makala hii imebaini kuwa katika mazingira ya kawaida kunaweza kuwa na washauri wengi ambao wanasukumwa kutaka kuwashauri watu wengine kwa namna tofauti. Hata hivyo, watu huogopa kuwashauri watu wengine kwa kuhofia kutopokelewa kwa ushauri wao au kubezwa kwa ushauri uliotolewa. Hali hii husababisha changamoto za mkengeuko wa malezi kuendelea kukua siku hadi siku kama ilivyo kwa mhusika Rosa ambaye aliamua kuendeleza tabia zake za umalaya.

#### 4.6 Matusi

Matusi ni maneno au matendo yanayoumiza na kujeruhi hisia, saikolojia na utu wa mtu yanayotolewa na mtu mmoja kwa mwingine au upande mmoja kwa upande mwingine (Archard, 2014). Matusi huweza kushusha hadhi ya mtu, kuondoa utu wake, thamani yake, hadhi yake, kunyanyasa na kuondoa heshima ya mtu (Ardener, 1973; Flynn, 1976; Nelson, 2011; Archard, 2014). Kwa jumla, matusi ni maneno, ishara au matendo ambayo hutolewa na mtu au kundi la watu dhidi ya mtu mwingine au kundi la watu na kuwafanya kujeruhiwa hisia zao, kukasirika, kuumiza saikolojia zao na kushusha utu wao, thamani yao, hadhi zao na kuwanyanyasa kwa namna tofauti. Katika riwaya ya *Rosa Mistika* mwandishi anamtumia mhusika Rosa na Zakaria kuonesha mkengeuko wa malezi kwa kutoa matusi. Mwandishi anaeleza:

Zakaria alifika nyumbani usiku kama kawaida yake. Alipofika Regina ndiye alikuwa wa kwanza kumjulisha kwamba Rosa alikuwa ndani. Zakaria aliguna tu na kusema, Rosa ndiye nani? Malaya hajawa mgeni wangu wala mtoto wangu.” Maneno haya yalisemwa kwa sauti na Rosa aliyasikia. Maneno haya yalimsumbua sana Rosa moyoni. Rosa hakujali kusikia maneno hayo yakisemwa na watu wengine. Lakini kusemwa na baba yake! Hili lilikuwa jambo kubwa sana... Rosa alilia... Rosa alikuwa amekwishakata shauri juu ya jambo hili. Alingoja kuchokozwa. Kweli Zakaria alichokoza mzinga wa nyuki. Rosa alitoka nje ghafla. Alikwenda karibu na baba yake. Alitapika maneno... “Kila wakati unatuchunga unafikiri utatua wewe!”... Maneno hayo yalimchoma moyoni Zakaria... Zakaria kutunza heshima yake, alifunua mdomo. Maneno fulani yalitoka mdomoni mwake. “Rosa

tangu leo wewe si mtoto wangu” “Tangu leo wewe si baba yangu”  
Rosa alidakia bila kukawia (Kezilahabi, 1971:57-58).

Katika dondoo hilo tunaoneshwa matusi ya Zakaria kwa Rosa na matusi ya Rosa kwa Zakaria baada ya Rosa kuchoka kuvumilia. Zakaria anamtukana Rosa kuwa ni malaya na kumkana kuwa si mtoto wake, jambo linalomuumiza Rosa. Maneno haya: “Rosa ndiye nani? Malaya hajawa mgeni wangu wala mtoto wangu”, nimatusi kwa Rosa na yanamuumiza na kumjeruhi sana. Rosa anatukanwa na baba yake kuwa ni malaya. Matusi haya yanamuumiza sana Rosa na kumfanyaaajione si sehemu ya mtoto ambaye anahaki ya kusikilizwa na kushauriwa kwa upole kuhusu changamoto zake za shuleni. Rosa anasikitika na kudhalilika kwa kusikia maneno ya matusi kama yale kutoka kwenye kinywa cha baba yake mzazi, Zakaria. Kitendo cha baba kumwita mtoto wake kuwa ni malaya hakikutarajiwa kwa Rosa na kwa jamii ya Rosa. Matusi ya Zakaria ndiyo yanayomuumiza Rosa kisaikolojia hadi kumfanya kulia machozi ya uchungu.

Jambo jingine linalojitokeza katika nukuu hiyo ni matusi ya Zakaria kumkana binti yake, Rosa, kuwa si mtoto wake. Kitendo hiki kinamsumbua sana Rosa kisaikolojia na kujihisi kunyanyaswa na kudharauliwa thamani yake na utu wake. Rosa anasukumwa kufikiri kuwa labda Zakaria si baba yake wa kumzaa kutokana na matusi hayo. Badala ya kupokelewa kwa upendo na furaha, Zakaria anampokea Rosa kwa matusi. Hali hii ndiyo inayomsukuma kutunza hasira ambazo hapo baadaye tunaoneshwa Rosa naye anashindwa uvumilivu na kumtukana baba yake, Zakaria.

Jambo la tatu linaloonekana katika nukuu hiyo ni mtoto kumtukana baba yake. Rosa ambaye ni mtoto anamtukana hadharani matusi Zakaria ambaye ni baba yake. Maneno “Kila wakati unatuchunga unafikiri utatuo wewe” yanayotolewa na Rosa kwa Zakaria katika nukuu hiyo ni matusi makubwa kwa Zakaria. Katika malezi ya Waswahili, baba mzazi hawezi kumuoa binti wa kumzaa yeye. Kwa hiyo, Rosa kumwambia baba yake Zakaria anamchungu ili amuo ni matusi makubwa. Maumivu ya matusi haya ndiyo yanayomsukuma Zakaria kumkana Rosa kwa mara ya pili kwa kusema: “Rosa tangu leo wewe si mtoto wangu.” Hata hivyo, Rosa naye anamkataa baba yake hadharani kwa kusema: “Tangu leo wewe si baba yangu.” Zakaria anamkataa Rosa kuwa si mtoto wake na Rosa naye anamkataa Zakaria kuwa si baba yake baada ya matusi wanayotukanana na kuwafanya kila mmoja kumia kwa upande wake. Rosa anajiona hana thamani kwa Zakaria kuwa mtoto wake.

Makala hii imebaini kuwa suala la matusi ni mkengeuko wa kimalezi kwa jamii. Wazazi wanapaswa kuwaongoza na kuwalea watoto wao kwa upole na maelekezo mema. Matusi yanapotolewa na wazazi kwa watoto wao huweza kusababisha maumivu na chuki kwa watoto dhidi ya wazazi wao. Hali hii inapotokea huweza kuwasukuma watoto kuchoka kuvumilia hali ya matusi na hivyo kuwafanya na wao kukengeuka kwa kuwajibu vibaya na kuwatukana wazazi wao. Ni vizuri kila upande unaohusika katika malezi uache matusi ili kuepusha

changamoto na athari zinazotokana na matusi kama ilivyokuwa kwa Rosa na Zakaria.

### 5.0 Hitimisho

Makala hii imefafanua na kuonesha mkengeuko wa malezi katika riwaya ya *Rosa Mistika*. Makala imeonesha namna wahusika katika riwaya hii wanavyoweza kutumiwa na mwandishi kuonesha kukengeuka kwa malezi na jinsi mkengeuko huo unavyosababisha migogoro kwa jamii wanamoishi. Mkengeuko huo wa malezi uliofafanuliwa ni pamoja na ubakaji, kujiua, rushwa, umalaya, kupuuza ushauri mwema na matusi. Makala imebaini kuwa mkengeuko wa malezi huwabadilisha wahusika na kuwa katika hali tofauti zinazowafanya wasikubalike katika jamii zao. Wahusika wanaokengeuka malezi wametumiwa katika riwaya hii ili kuonesha uhalisia wa matukio hayo katika jamii na kuwa matukio hayo ya mkengeuko wa malezi yapo katika jamii. Lengo kubwa ni kuifanya jamii iamke na kuchukua hatua za mabadiliko ili kujenga jamii mpya.

### Marejeleo

- Archard, D. (2014). "Insults, Free Speech and Offensiveness." *Journal of Applied Philosophy*. 31(2): 21-141.
- Ardener, S.G. (1973). "Sexual Insult and Female Militancy." *Man Sep 1973, New Series*. 8 (3): 422-440.
- Baker, K.K. (1999). "What Rape is and What it Ought not to be." *American Bar Association*. 39(3):233-244.
- BAKITA (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers Ltd.
- BAKIZA (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.
- Beebee, T.O. (2016). *The Ethics of World Literature*. Pennsylvania. The Pennsylvania State University.
- Belsky, J. (1984). "The Determinant of Parenting: A Process Model." *Child Development*. 55(1): 83-96.
- Belle, J.L. (2017). "Factors that Influence Student Behaviour in Secondary School." *European Journal of Educational and Development Psychology*. 5(5):27-36.
- Bownlee, C. (2006). "Nurture Takes Spotlight." *Science News*. 169(25):392-393,396.
- Carter, M.J. na Carter, S. (2014). "How Themes in Literature can Inform Sociological Theory, Research and Teaching." *Springer Science and Business Media*. 45(4): 388-411.
- Chatterjee, K.K. (1988). "Lukacs on Tagore: Ideology and Literary Criticism." *Sayika Academy Indian Literature*. 31, 3(125): 153-160.
- Coser, L. (1963). *Sociology through Literature: An Introductory Reader*. Englewood Cliffs: Prentice Hall.

- Curzer, H.J. (1996). "Aristotle's Bad Advice about Becoming Good." *Philosophy*. 71(275): 139- 146.
- Diegner, L. (2002). "Allegories in Euphrase Kezilahabi's Early Novels." *Swahili Forum IX*.43-74.
- Doepke, M. na Zilibotti, F. (2019). "The Economic Roots of Helicopter Parenting." *The Phi Delta Kappan*. 100(7): 22-27.
- Dubey, A. (2013). "Literature and Society." *Journal of Humanities and Social Science*. 9(6):84-85.
- Duric, M. na Bunijevac, M. (2017). "Parental Involvement as an Important Factor for Successful Education." *C.E.P.S Journal*. 7(3):137-153.
- Farley, M. (1994). "Prostitution: The Oldest Use of Abuse of Woman." *Off Our Backs Inc*. 24 (5):14-22.
- Flynn, C.P. (1976). "Sexuality and Insult Behaviour." *The Journal of Sex Research*. 12 (1):1-16.
- Hellen, G.C. (1966). "Sociology of Literature." *Pi Gamma Mu*. 41 (1):12-18.
- Iyer, K.P. (1998). "Prostitution: A Feminist Ethical Analysis." *Journal of Feminist Study in Religion*. 14 (2):19-44.
- Jonas, M. (2017). "Resentment of Advice and Norms of Advice." *Ethical Theory and Moral Practice*. 20(4):813-828.
- Joseph, A. (1994). "Good Advice." *Callaloo*. 17 (2): 462-463.
- Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. Dar es Salaam: East African Literature Bureau.
- Kezilahabi, E. (1973). *Dunia Uwanja wa Fujo*. Dar es Salaam: EALB.
- Kezilahabi, E. (1974). *Kichwamaji*. Dar es Salaam: EAPH.
- Kezilahabi, E. (1979). *Gamba la Nyoka*. Dar es Salaam: EAP.
- Madumulla, J.S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historiana Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Limited.
- Mahonge, F.R. (2016). *The Representation of Masculinity in Euphrase Kezilahabi's Novels*. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Moi.
- Martin, C. (2017). "Parenting as a Public Problem in a Neoliberal Era: A Changing Regime in France?" *Journal of Comparative Family Studies*. 48(3):303-314.
- Mayaka, G. (1991). *Ukengeushi wa Wasomi katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Mbatiah, M. (1997). "Mienendo Mipya katika Uandishi wa Kezilahabi: *Nagona na Mzingile*" *Mulika*. 24:1-11.
- Mbatia, M. (1996/97). "Maana na Matumizi ya Upambanyaji: Tahakiki ya *Rosa Mistika*." *Kioo cha Lugha*. 2:61-70.
- Mbatiah, M. (2012). "Riwaya ya Kiswahili kama Tahakiki ya Jamii Baada-Ukoloni." *Kioo cha Lugha*. 10:95-101.

- Mbatiah, M. (2016). *Riwaya ya Kiswahili: Chimbuko na Maendeleo yake*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- McCall, R.B. (1981). "Nature-Nurture and the two Realms of Development: A Proposed Integration with Respect to Mental Development." *Child Development*. 52(1):1-12
- Mitchel, P. (2010). "Helicopter Parents." *Children's Voice: Child Welfare League of America. Children's Voice*. 19(6): 33.
- Mlacha, S.A.K. (1985). "Dhima ya Methali katika Malezi." *Kiswahili*. 51(1) na 52(2):176-186.
- Mlacha, S.A.K. (1986). "The Identification of Personality Differences in Kiswahili Prose Fiction." *Kiswahili*. 49:146-169.
- Mlacha, S.A.K. (1989). "The use of Metaphors in Kezilahabi's Novel: Rosa Mistika." *Kiswahili*. 40: 25-31.
- Moen, O.M. (2014). "Is Prostitution Harmful?" *Journal of Medical Ethics*. 40(2):73-81.
- Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.
- Nelson, J.L. (2011). "Hurts, Insults and Stigmas: A Comments of Murphy." *Journal of Medical Ethics*. 37(3): 66-67.
- Nworah, A.G na Eziaba, N.C. (2014). *Literature, Society and the Writer in Tripartite Unity*. Canberra. Australian International Academic Centre.
- Plomin, R. na Asbury, K. (2005). "Nature and Nurture: Genetic and Environmental Influences on Behaviour". *The Annals of America Academy of Political and Social Science*. 600: 86-98.
- Salari, R; Wells, M. na Sarkadi, A. (2014). "Child Behavior, Parenting Behavior and Parental Adjustment in Mothers and Fathers in Sweden." *Scandinavian Journal of Public Health*: 42(7):547-553.
- Sanga, D. (2018). "Moral Panic: Hidden Stories of Kangamoko Dancers in Dar es Salaam –Tanzania." *Kioo cha Lugha*. 16: 81-94.
- Seaver, P. (2009). "Suicide." *The Furrow*. 60(3):172-175.
- Shleifer, A. na Vishny, R.W. (1993). "Corruption". *The Quarterly Journal of Economics*. 108(3):599-617.
- Small, M.L na Pager, D. (2020). "Sociological Perspective on Racial Discrimination." *The Journal of Economic Perspective*. 34 (2): 49-67.
- Titus, S. (2018). *Georg Lukas. The Standard Encyclopedia of Philosophy*. Palo Alto. Stanford University Press.
- TUKI (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- Wanjala, M. (2015). *Usawiri wa Malezi Unavyoathiri Utambulisho wa Vijana katika Riwaya ya Kiswahili*. Tasnifu ya Umahiri (Haijchapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.